*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 70-91*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Tafsiri kama Nyenzo ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni: Mfano wa Kiswahili Nchini Uganda

*Sarah Ndanu M. Ngesu[1] na George Yesse Mrikaria*

## Ikisiri

Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda unachukua mwelekeo wa ufundishaji wa lugha ya kigeni kwa sababu wajifunzaji hawapati ingizo kutoka katika jamii. Lengo la makala hii ni kuchunguza tafsiri kama nyenzo ya ufundishaji wa lugha ya kigeni nchini Uganda. Madhumuni yake ni kuonesha kwamba ingawa tafsiri hupingwa na baadhi ya wataalamu katika ufundishaji wa lugha ya kigeni, ina nafasi yake na haiwezi kuepukika katika miktadha maalumu kama ilivyo nchini humo. Makala inaibua hoja kwamba tafsiri inayotumika katika ufundishaji wa Kiswahili ni ya kimawasiliano ambayo ni tofauti na tafsiri-sarufi inayojiegemeza kutafsiri kaida za lugha. Ili kufikia lengo la makala hii, data ilikusanywa kwa njia ya hojaji kutoka kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili waliokuwa wakisoma Kiswahili katika shule za sekondari jijini Kampala. Wengi wa wanafunzi hao walianza kusoma Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza, yaani hawakusoma Kiswahili shule ya msingi. Nadharia ya Umotishaji Lugha ilitumika kuchanganua data za makala hii ambayo imezingatia maboresho yaliyofanywa na Dörnyei (1994). Matokeo yanaonesha kwamba tafsiri ya kimawasiliano hutumika katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda katika shule za sekondari. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa tafsiri hutumika kama nyenzo ya ufundishaji kwa lengo la kuwapa motisha wajifunzaji katika mazingira ambayo hawapati ingizo kutoka kwa jamii.

[1] Mhadhiri, Idara ya Isimu, Lugha na Fasihi, Kitivo cha Elimu, Insia na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha South Eastern, Kitui, Kenya. Baruapepe: sarahngesu@gmail.com, sngesu@seku.ac.ke

Mrikaria ni Mhadhiri, Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: gmrikaria@gmail.com

**1.0 Usuli wa Tafsiri katika Ufundishaji wa Lugha za Kigeni**

Tafsiri ilianza kutumika katika ufundishaji wa lugha katika karne ya kumi na nane wakati lugha za Kiyunani na Kilatini zilipokuwa zinafundishwa shuleni (Omar, 2019). Tafsiri-sarufi ilikuwa maarufu na ilitambulika kuwa mbinu rasmi. Wataalamu wa ufundishaji wa Kiyunani na Kilatini katika shule za Ujerumani kama vile Carl Julius Ploetz, Johann Heinrich Philipp Seidenstücker, Johann Valentin Meidinger na Heinrich Gottfried Ollendorff, walitumia tafsiri-sarufi kufundishia lugha hizo kuanzia mwaka 1783 hadi 1849 (Marques na Solís-Becerra, 2013). Marques na Solís-Becerra (2013) wanaeleza kwamba tafsiri-sarufi ni mbinu ya ufundishaji iliyoasisiwa na wataalamu wa Kijerumani na baadaye kuendelezwa na wanaisimu wa Marekani. Kwa mujibu wa Siefert (2013), mbinu ya tafsiri-sarufi iliasisiwa na Meidinger mwaka 1783 na kuendelezwa na wafuasi wake wanne: Johann Seidenstücker, Frauz Ahn, Heinrich Gottfried Ollendorff na Karl Ploetz, ambao walikuwa wataalamu wa taaluma ya ufundishaji wa lugha.

Katika karne ya kumi na tisa walimu wa Kiingereza pia walitumia tafsiri-sarufi kufundishia Kiyunani na Kilatini. Lengo kuu la matumizi ya tafsiri-sarufi lilikuwa kufundisha lugha kwa kutafsiri kaida na msamiati wa lugha lengwa (kuanzia sasa, LL) yaani lugha inayofundishwa (Hull, 2018). Wanafunzi walitakiwa kutumia mkakati wa tafsiri sisisi ili kuimarisha uwezo wao wa kusoma, kuandika pamoja na kutafsiri kazi za kifasihi (Machida, 2011). Kwa mujibu wa Ivanova (2016) na Hull (2018), mbinu ya tafsiri-sarufi, kwa muda mrefu iliendelea kuwa na umaarufu kuliko mbinu nyingine za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni (kuanzia sasa, LgK) na wa lugha bora au lugha rasmi[2] kuanzia miaka ya 1840 hadi 1940. Baadaye tafsiri ilitumiwa kufundishia lugha za kisasa na hata hivi leo katika maeneo mengi duniani, kama vile Uchina, India, Pakistani, Urusi na Hispania mbinu hii hutumika kwa upana katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK (Marques na Solís-Becerra, 2013).

Hata hivyo, mbinu ya tafsiri-sarufi iliyotumiwa katika mchakato wa ufundishaji ilizua mijadala mikali kutokana na baadhi ya wanazuoni kupinga matumizi yake (Siefert, 2013; Ayvazyan, 2017). Mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, kundi la wanazuoni waliojitambulisha kama wanamageuzi[3] lilipinga matumizi ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji wa lugha (Ngesu, 2021). Wanamageuzi hao waliongozwa na Wilhelm Viëtor kuanzia mwaka wa 1850 hadi 1918. Viëtor alitilia mkazo lugha ya mazungumzo, hususani fonetiki kuliko lugha ya maandishi. Hivyo, mbinu ya moja kwa moja ilianza kutumiwa badala ya tafsiri-sarufi katika miaka ya 1900 (Kelly &

---

[2] Tafsiri ya kirai '*Classical languages*'; Mgullu (2001:15) anaeleza kwamba lugha rasmi ni mtindo wa lugha ambao mara nyingi ulitumiwa na watu mashuhuri na ukaaminika kuwa ni mtindo bora na ambao unafaa kuigwa na wengine. Massamba (2013:11) anatumia '*lugha bora*' na kueleza kwamba ni lugha ambayo husemekana kuwa ndiyo iliyokuwa bora katika wakati huo na ambayo ilitumiwa (na pengine huendelea kutumiwa) kama kigezo cha ubora wa lugha.

[3] Hawa ni wataalamu wa mageuzi (*Reform Movement*) waliopinga matumizi ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji wa lugha za kigeni.

Bruen, 2015). Mbinu hii ilianza kuwa maarufu huko Ujerumani na Ufaransa. Mbinu nyinginezo zilizohusiana na mbinu ya moja kwa moja zilianza pia kuibuka. Kwa mfano, mkabala wa kimawasiliano ulichangia kwa kiasi kikubwa kupuuzwa kwa tafsiri-sarufi katika ufundishaji wa lugha na hata leo mkabala huu unapendekezwa kuwa bora katika ufundishaji wa lugha. Wanamageuzi wengine waliopinga matumizi ya tafsiri-sarufi ni Passy (1899), Sweet (1900), Bloomfield (1933), Celce-Murcia na Rosensweig (1979), Howatt (1984), Omaggio (2001), Brown (2007) na Doff (2008).

Wataalamu hawa walidai kwamba mbinu ya tafsiri-sarufi haitilii maanani vipengele vitatu muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha: stadi ya kuzungumza, uzingativu wa muundo wa lugha na mbinu changamani za mawasiliano (Vermes, 2010). Pia, walidai kwamba tafsiri-sarufi haina uhalisia kwa kuwa huegemea stadi za kusoma na kuandika na kwamba mjifunzaji hutegemea lugha yake ya kwanza inayoathiri ujifunzaji wake wa LgK. Aidha, walidai kwamba matumizi ya tafsiri-sarufi hayawasaidii wajifunzaji kufanya mazoezi ya kuwasiliana kwa kutumia LL.

Hata hivyo, wanaopinga matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha wanaonekana kuegemea katika kuhusisha tafsiri na mbinu ya tafsiri-sarufi. Wataalamu hawa hawatofautishi tafsiri-sarufi na tafsiri kama mbinu ya ufundishaji wa LgK (tafsiri kimawasiliano) katika kurahisisha mawasiliano baina ya mwalimu na mjifunzaji. Dhana hizi hutofautiana kutegemea uamilifu, hadhira, lengo na mwasilishaji wa ujumbe (Cook, 2018). Kwa mfano, tafsiri kama nyenzo ya ufundishaji wa LgK hutumiwa kurahisisha mawasiliano, kukuza umilisi na kutathmini uelewa wa mjifunzaji. Tafsiri-sarufi iliyotumiwa katika ufundishaji wa Kiyunani na Kilatini ilijikita katika tafsiri za matini kwa kuzingatia kaida za LL. Pia, wanaopinga wana maoni yanayojielekeza katika tafsiri ya matini na kukosa kuitambua tafsiri kama mchakato wa mawasiliano darasani. Lengo kuu la matumizi ya tafsiri-sarufi lilikuwa kuwasaidia wafundishaji na wajifunzaji kuelewa muundo na sarufi ya lugha. Aidha, mbinu hii ilihusu uchanganuzi wa matini bora kileksika na kisarufi na ilionekana kama hatua ya kuboresha mbinu ya kimapokeo ya Kiskola[4] iliyokuwapo awali. Pia, tafsiri-sarufi ilitumika mara nyingi katika uchanganuzi wa matini za kifasihi ili kuwatayarisha wajifunzaji kuwa wasemaji bora na kama kigezo cha kuwatenganisha wanafunzi mahiri na wasio mahiri. Matumizi ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji wa Kiyunani na Kilatini ni tofauti na matumizi ya tafsiri kama njia ya kurahisisha mawasiliano katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK katika karne ya ishirini na moja.

Kutokana na mageuzi yaliyofanywa na wanamageuzi kama vile Viëtor (1882), Passy (1899), Sweet (1900) na Bloomfield (1933), tafsiri-sarufi iliondolewa katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK na/au Lg2. Mkabala wa moja kwa moja na

[4]'Kiskola' ni tafsiri ya mtafiti ya '*Scholastic Method*'. Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu dhana hii imetumika kuelezea mbinu ya ufundishaji iliyokuwa ikitumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kabla ya mbinu ya tafsiri-sarufi.

mkabala wa kimawasiliano ulianza kutumiwa na kuendelea kwa miongo mingi iliyopita (Cook, 2010, 2018). Mbinu ya mawasiliano inasisitiza umuhimu wa wanafunzi kuwa na umilisi wa kimawasiliano pamoja na uwezo wa kueleweka kwa wazawa wa lugha wanayojifunza.

Hata hivyo, matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha yanarejea kwa kasi katika karne ya ishirini na moja kutokana na kuongezeka kwake katika ufundishaji wa LgK (Cook, 2018; Karimah, 2020). Tangu miaka ya 1980 kumekuwa na mijadala endelevu kuhusu kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha (Ngesu, 2021). Waandishi mbalimbali kama Cook (2010, 2018), Leonardi (2010), Dagilienė (2012), Laviosa (2014), Abdul-Azim (2017), Barnes (2018), Panda (2018), Anwar (2019), Ngesu (2020, 2021) wameendelea kuandika ili kutetea kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK bila kufikia makubaliano.

Merç (2019) anaeleza kwamba mbinu ya tafsiri kwa ujumla katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha inahusishwa na matumizi ya lugha ya kwanza (kuanzia sasa, Lg1) katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK na lugha ya pili (kuanzia sasa, Lg2). Hata hivyo, katika utafiti wa Ngesu (2021) imebainika kwamba katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda, tafsiri hutumika baina ya Lg2 (Kiingereza) na Lg2/LgK (Kiswahili). Katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu na mjifunzaji hutumia tafsiri ya mazungumzo na tafsiri ya maandishi. Tafiti za awali kuhusu tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda (taz. Ngesu, 2020) zilijiegemeza kupata data kutoka kwa walimu wanaofundisha Kiswahili pekee ingawa mchakato wa ufundishaji huhusisha mwalimu na mwanafunzi. Makala hii imelenga wajifunzaji kama watoataarifa ili kuibua matokeo yanayoweza kuchangia maarifa zaidi katika suala hili.

### 1.1 Hali ya Sasa ya Tafsiri katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha za Kigeni

Tafiti mbalimbali (taz. Nida, 1998; Vermes, 2010; Machida, 2011; Ito, 2017; Cook, 2018; Mahi, 2018; Fitori, 2019; Pym, 2019; Karimah, 2020, Ngesu, 2020 na 2021) zinaonesha kwamba licha ya kupingwa kwa matumizi ya tafsiri-sarufi katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK, mbinu ya tafsiri imeendelea kutumiwa na walimu, wanafunzi na wachapishaji. Tafiti hizi pia zinaonesha kuwa tafsiri ndiyo mbinu inayotumika zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK na/ au Lg2. Marinac na Baric (2018) wanaeleza kwamba katika nchi ambazo tafsiri hutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kama vile China, India na Urusi wajifunzaji huwa na umilisi wa hali ya juu wa lugha wanayojifunza. Vilevile, imebainika kwamba katika baadhi ya nchi ambazo tafsiri haitumiwi kufundisha LgK, umilisi wa wajifunzaji ni wa kiwango cha chini. Hivyo, wanadai kwamba tafsiri ni mbinu muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK ikitumiwa kama mbinu mojawapo badala ya kutumiwa kama mkabala wa pekee kama ilivyotumiwa mbinu ya tafsiri-sarufi.

Pia, imedhihirika kuongezeka kwa machapisho kuhusu kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK (Cook, 2018). Wataalamu kadhaa wamejitokeza kuitetea na kuonesha umuhimu wake katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK hususani lugha za Ulaya. Wataalamu Duff (1989), Albir (1994), Klaudy (2003), Cook (2010, 2013, 2018), Vermes (2010), Laviosa (2014) na Ngesu (2018) wanakubaliana kwamba tafsiri ni nyenzo inayowasaidia wajifunzaji kuelewa maneno na dhana za LL. Wanaendelea kudai kwamba tafsiri ina nafasi kubwa katika elimu ya uwililugha na inajitegemea kama taaluma ya kiakademia. Tafsiri imeanza kujitokeza kama shughuli ya kimawasiliano tofauti na tafsiri-sarufi. Kwa mfano, tarehe 9/9/2019 kulikuwa na kongamano la tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha jijini Cambridge nchini Uingereza. Tangazo hili lilitolewa tarehe 25/6/2019 na lilieleza hivi:

> *Conference on translation in language teaching and learning. Title: The Translation Turn: Current Debates on the Role of Translation in Language Teaching and Learning. Venue: Runcie Room, Faculty of Divinity, Sidgwick Site, West Road, Cambridge CB3 9BS. Translation in language teaching is currently undergoing a process of reassessment and revival. The increasingly diverse linguistic background of todays populations has led to new needs and challenges in foreign language classroom. Thus, the strict monolingualism in the target language that became dogma in the latter part of the 20th Century has been replaced today by bi, multi- and plurilingual approaches.*
>
> **Chanzo:** Lucia Pintado (2029) lucia.pintado@dcu.ie
>
> Kongamano kuhusu tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Mada: Mabadiliko katika Tafsiri: Mijadala kuhusu Nafasi ya Tafsiri katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha. Mahali: Chumba cha Runcie, Shule ya Divinity, Sidgwick Site, West Road, Cambridge CB3 9BS. Kwa sasa tafsiri katika ufundishaji wa lugha iko katika mchakato wa kufanyiwa tathmini na kuhuishwa katika ufundishaji wa lugha. Hali ya wingilugha duniani imechangia mahitaji mapya na changamoto mpya katika darasa la LgK. Hivyo, nafasi ya mbinu ya lugha moja iliyotawala ufundishaji wa LgK mwishoni mwa karne ya 20 imechukuliwa na mikabala ya lugha mbili au lugha zaidi ya mbili ambapo tafsiri inapaswa kutumika katika muktadha huu (Tafsiri ya waandishi).
> **Chanzo:** Lucia Pintado (2029) lucia.pintado@dcu.ie

Kwa kurejelea dondoo hili, inadhihirika kwamba tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK kwa sasa haiwezi kuepukwa kufanyiwa utafiti. Hinga (2010) anaeleza kwamba lugha ya Kiingereza hutumiwa nchini Kenya kuwasaidia

wanafunzi kujifunza lugha ya Kijerumani. Anaongezea kwamba umilisi wa Kiingereza walio nao wanafunzi huwasaidia kujifunza Kijerumani nchini Kenya. Jambo hili linaungwa mkono na Ito (2017) na Karimah (2020) wanaoshadidia kwamba tafsiri haiwezi kuepukwa katika ujifunzaji wa LgK.

Hivyo, inadhihirika kwamba licha ya kupingwa kwa matumizi ya tafsri katika ufundishaji wa LgK kutokana na uhusiano wake na tafsiri-sarufi, tafsiri imeendelea kutumiwa katika maeneo mbalimbali duniani. Panda (2018) anaeleza kwamba tafsiri hutumiwa katika ufundishaji wa Kiingereza, Kihindi na Kisanskriti nchini India. Aidha, Liu (2019) anaeleza kwamba tafsiri hutumiwa katika shule, vyuo na vyuo vikuu vinavyofundisha Kiingereza kama LgK nchini China. Wakishadidia hali hii, Pym (2019) na Karimah (2020) wanaeleza kwamba tangu miaka ya 2000 kumekuwa na ongezeko la machapisho kuhusu kurejeshwa kwa tafsiri katika ufundishaji wa LgK. Tafsiri imeanza kujitokeza kama shughuli ya kimawasiliano tofauti na tafsiri-sarufi iliyopingwa na kuzua mjadala endelevu. Pintado (2019) anadai kwamba hata kama tafsiri imepuuzwa katika mitaala lakini inatumika katika shughuli halisi za ufundishaji na ujifunzaji wa LgK.

Nchini Uganda, tafsiri baina ya Kiswahili na Kiingereza hutumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili (Ninsiima, 2017). Pia, tafsiri hutahiniwa kama kipengele kimojawapo cha lugha ya Kiswahili katika mitihani ya kidato cha nne na cha sita (Masengo, 2018). Ili kukabiliana na changamoto za kutafsiri, vipengele vya lugha darasani, walimu hutumia tafsiri na mikakati mbalimbali ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili. Vilevile, Jjingo na Visser (2017) wanaeleza kwamba hata kama taasisi inayohusika na mitihani nchini Uganda imekuwa ikitahini somo la Kiswahili, Kiswahili hakikuwa kikifundishwa katika shule nyingi nchini Uganda. Hali hii imechangia kutokuwapo kwa mbinu mwafaka za ufundishaji wa Kiswahili. Naye Mtesigwa (2009) anaeleza kwamba hali ya kutokuwa na mbinu mwafaka za ufundishaji wa Kiswahili imechangia mbinu za zamani kutumika katika ufundishaji wa Lg2 na LgK. Mbinu mojawapo inayozungumziwa ni tafsiri. Walimu wengi wanaofundisha Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda, kama ilivyo katika vyuo vikuu vingi katika ukanda wa Afrika Mashariki, wanatumia tafsiri kufundishia ijapokuwa haitambuliwi katika mtaala.

Kwa hivyo, makala hii imechochewa na tatizo la kinadharia na pengo la maarifa. Tatizo la kinadharia linatokana na matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda kinyume na mbinu ya kimawasiliano inayopendekezwa na wataalamu wa ufundishaji wa LgK. Pengo la maarifa linatokana na uhaba wa tathmini ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK. Vilevile, tafiti tangulizi (Ngwendu, 2016; Ito, 2017; Mahi, 2018; Fitori, 2019; Karimah, 2020) kuhusu tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha zilichunguza lugha tofauti zisizo na mnasaba na Kiswahili licha ya kuwa matumizi ya tafsiri hutofautiana kulingana na lugha husika na muktadha wa matumizi. Aidha, tafiti chache kuhusu tafsiri na ufundishaji wa Kiswahili (Philipo, 2016, 2017; Ngesu, 2020) zimejielekeza kupata maoni ya walimu bila kuwahusisha wajifunzaji. Hivyo, inaonekana kwamba

kuna haja ya kuchunguza maoni ya wajifunzaji kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ili kubaini mielekeo yao.

## 2.0 Methodolojia

Makala hii ilihusisha uchambuzi wa nyaraka, yaani kazi za wanafunzi za mazoezi ya darasani yaliyofanywa kwa vipindi viwili na hata za baadaye katika kila darasa. Kazi hizo zilihusu mada mbalimbali. Matumizi ya mbinu hii yaliwawezesha watafiti kubaini tafsiri ya vipashio vya lugha katika ujifunzaji wa Kiswahili. Pia, mbinu ya hojaji ilitumiwa kwa ajili ya kupata taarifa kutoka kwa wajifunzaji ili kupata taarifa kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili. Uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Umotishaji Lugha kwa mujibu wa Dörnyei (1994). Nadharia hii ina mihimili mitatu; mhimili ulioongoza uchanganuzi wa data ni wa kwanza unaohusu umotishaji unaotokana na somo au kozi. Umotishaji huu unahusu muhtasari wa somo/kozi unaotumiwa, vitendeakazi, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, na shughuli za darasani.

## 3.0 Hali ya Ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda

Hali ya kuchangamkia ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda imetokana na umuhimu na dhima ya Kiswahili kikanda na kimataifa (Masengo, 2018; Ngesu, 2021). Aidha, kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mtazamo chanya wa Serikali ya Uganda kwa sasa kuhusu Kiswahili umechangia kuwapo kwa mwamko mpya kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Kwa mujibu wa Majariwa (2014), Serikali ya Uganda inajitahidi kuweka taratibu za kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini humo ili kuwa katika kiwango kimoja na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa maelezo katika Muhtasari wa Ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda, lengo kuu la ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini humo limechochewa na mambo manne. Kwanza, Kiswahili ni lugha ya mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na mojawapo ya lugha chache za Afrika ambazo zinazungumzwa katika maeneo mengine duniani. Pili, Kiswahili ni moja ya lugha zinazoonesha maendeleo makubwa na ya kasi duniani. Tatu, Kiswahili ni mojawapo ya lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwisho, serikali ya Uganda inatambua umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya kikanda na kimataifa inayoweza kuwaunganisha wananchi wa Uganda.

Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda umechochewa vilevile na hali ya kiisimu ya Uganda ya wingilugha na umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna lugha zaidi ya 43 za asili nchini Uganda na wanafunzi huzungumza lugha moja au mbili kati ya hizo. Kiingereza hutumiwa kufundishia masomo yote kutoka darasa la nne (shule za msingi) hadi kidato cha sita na chuo kikuu. Kiingereza pia ni somo la lazima na kina hadhi ya lugha ya tabaka la juu pamoja na la wasomi (Masengo, 2018). Pia, wanafunzi hujifunza Kiingereza kama Lg2 kabla ya Kiswahili kinachofundishwa kama LgK. Masengo anaeleza kwamba mwanzoni ni shule chache


sana zilizokuwa zinafundisha somo la Kiswahili. Kufikia sasa, Kiswahili hufundishwa katika shule chache vijijini na mijini kutoka kidato cha kwanza hadi cha sita. Katika ngazi ya chuo kikuu, Kiswahili hufundishwa kama somo la hitiari kwa wanafunzi wanaosomea digrii ya ualimu. Katika hali hii, wanafunzi wanaosoma Kiswahili huwa wana uwingilugha baina ya lugha zao za asili na Kiingereza.

Katika utafiti wa Jjingo (2011), asilimia 75 ya watoataarifa walikiri kwamba Kiswahili ni lugha ya Afrika Mashariki na kuna umuhimu wa kuwa na lugha moja ya kuwaunganisha wanajamii wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo, kuna haja ya kukuza na kuendeleza Kiswahili ili kuimarisha utangamano na wananchi wa nchi nyingine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jjingo (2011) aliwahoji wananchi ambao walielezea kwamba Kiswahili hakizungumzwi nchini Uganda kama anavyosisitiza:

> *However, only 25% of the interviewees admitted that in Uganda, Kiswahili hardly operates and no Ugandan can speak that language* (Jjingo, 2011:69).
>
> Hata hivyo, ni 25% tu ya wasailiwa wote waliokiri kwamba nchini Uganda Kiswahili kinatumika na hakuna Mganda anayeweza kuzungumza lugha hiyo (Tafsiri ya waandishi).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili haizungumzwi na wanajamii wengi nchini Uganda. Hata hivyo, wananchi wengi wa Uganda wanakubali kwamba njia muhimu ya kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini humo ni kuhakikisha inafundishwa katika ngazi zote kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu (Jjingo, 2011).

Jjingo na Visser (2017) wanaeleza kwamba Uganda imejaribu kusisitiza ufundishaji wa Kiswahili kwa miaka mingi bila mafanikio makubwa. Aidha, wanaeleza kwamba mapendekezo mengi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili yamesalia katika machapisho. Halikadhalika, Jjingo na Visser (2018) wanaeleza kuwa Kiswahili kimeendelea kuchukuliwa kama LgK nchini Uganda licha ya kupendekezwa kuwa lugha rasmi ya pili. Aidha, utafiti wa Ngesu (2021) unaonesha kwamba wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari jijini Kampala hawapati ingizo katika jamii. Miongoni mwa wajifunzaji 288 waliojibu swali la lugha wanazozungumza wakiwa nyumbani, majibu ya wajifunzaji walio wengi yalionesha kuwa hawazungumzi Kiswahili wakiwa nyumbani kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1:




***Kielelezo Na. 1: Lugha ambayo wajifunzaji huzungumza wakiwa nyumbani***
**Chanzo:** Ngesu (2021:160)

Kielelezo Na. 1 kinaonesha kwamba kwa ujumla asilimia kubwa, yaani 90% ya wajifunzaji (65%, wanazungumza lugha nyingine na 25% wanazungumza Kiingereza) hawazungumzi Kiswahili wakiwa nyumbani. Hivyo, hali hii huifanya lugha ya Kiswahili kuwa ngeni kwa wajifunzaji. Wataalamu wa taaluma ya ujifunzaji wa lugha za kigeni kama vile Panda (2018) na Liu (2019), wanasisitiza kwamba ingizo linalotokana na kutangamana na wanajamii wanaozungumza lugha lengwa ni muhimu katika kukuza umilisi wa LgK. Lengo muhimu la kujifunza lugha ni kuweza kuwasiliana ambalo ni dhihirisho kubwa la ufanisi katika ujifunzaji wa lugha. Lengo hili linaweza kufikiwa iwapo wajifunzaji wa lugha wanapata nafasi ya kufanyia mazoezi walichojifunza darasani, yaani kuzungumza na wanajamii nje ya darasa. Imebainika kwamba wajifunzaji wa Kiswahili jijini Kampala hawapati nafasi hii kwa kuwa hawazungumzi Kiswahili wakiwa nyumbani.


Uchanganuzi wa majibu ulifanywa kutegemea wanafunzi wa kila shule kutoka shule saba zilizoshiriki. Matokeo yanaoneshwa katika Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Maoni ya Watoataarifa (wanafunzi) kuhusu Kiwango cha Watu Wanaozungumza Kiswahili nchini Uganda**

| Na. | Shule | Jumla ya Watoataarifa | Watu Wengi | Watu Wachache | Watu Wachache sana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shule ya Kampala | **51** | 17 | 25 | 9 |
| 2. | Shule ya Kawempe Muslim | **71** | 13 | 48 | 10 |
| 3. | Shule ya Kibuli | **48** | 13 | 31 | 4 |
| 4. | Shule ya Lubiri | **52** | 12 | 29 | 11 |
| 5. | Shule ya Midland | **29** | 11 | 15 | 3 |
| 6. | Shule ya Muyenga | **16** | 7 | 7 | 2 |
| 7. | Shule ya Progressive Kitintale | **21** | 4 | 15 | 2 |
| **JUMLA** | | **288** | **77** | **170** | **41** |

**Chanzo:** Ngesu (2021:161)

Data katika Jedwali Na.1 inaonesha kwamba kati ya wanafunzi 288, wanafunzi 170 (59%), walisema Kiswahili ni lugha ya watu wachache. Wanafunzi 77, sawa na 27%, walisema ni lugha ya watu wengi na wanafunzi 41, sawa na 14%, walisema ni lugha ya watu wachache sana. Kielelezo Na. 2 kinaonesha mchanganuo kwa asilimia kama ilivyoelezwa:




***Kielelezo Na. 2:*** ***Maoni ya watoatarifa (wanafunzi) kuhusu kiwango cha watu wanaozungumza Kiswahili nchini Uganda***

**Chanzo:** Ngesu (2021:161)

Kwa kurejelea Kielelezo Na. 2, wanafunzi 59% waliosema Kiswahili ni lugha ya watu wachache, wakiongezwa wanafunzi 14% waliosema Kiswahili ni lugha ya watu wachache sana, inadhihirika kwamba jumla ya 73% ya wanafunzi wana maoni kwamba Kiswahili ni lugha ya watu wachache nchini Uganda. Hii ina maana kwamba wajifunzaji wengi wa Kiswahili hawapati ingizo nyumbani wala katika mazingira ya jamii nje ya darasa. Katika muktadha kama huo, wataalamu Panda (2018) na Liu (2019) wanakubaliana kwamba tafsiri ina manufaa makubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa LgK. Hivyo, mikakati ya tafsiri kama vile ubadilishaji kategoria, ubadilishaji mtazamo, na tafsiri sisisi iliwasaidia kutumia umilisi walio nao wa Lg2 (Kiingereza) ili kujifunza Kiswahili (LgK).

Hali ya Kiswahili kuwa kama LgK nchini Uganda inachangia matumizi ya tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ambayo wajifunzaji huielewa barabara hususani katika shule za sekondari jijini Kampala. Kama ilivyoelezwa awali, Kiingereza ni lugha rasmi nchini Uganda na wanafunzi hujifunza lugha hii kutoka

shule za msingi. Hata hivyo, mapitio ya maandiko yanadhihirisha kwamba tafsiri haitambuliwi kama njia ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda licha ya kuwa inatumika kwa kiwango cha juu. Kwa mfano, Muhtasari wa Kiswahili nchini Uganda uliokuwa ukitumika wakati wa utafiti huu unatoa kipaumbele kwa mbinu kama vile chemshabongo, majadiliano, maigizo, ujifunzaji wa kimakundi, uvumbuzi elekezi, na ushirikishaji wa wajifunzaji wawiliwawili kama inavyooneshwa katika dondoo lifuatalo lililonukuliwa katika Muhtasari wa Kiswahili (2008/2013/2016: ix):

> ***HOW TO USE THIS SYLLABUS:*** *In this syllabus, teaching and learning strategies have been suggested. However, a teacher is expected to use his/her discretion to pick and if necessary, blend certain aspects of methodology to enhance teaching. Methods and their procedures have been suggested in this syllabus to enable the teacher interpret the syllabus easily. Some of the methods suggested include: brainstorming, discussion, role-play, circus, cooperative learning, jig-saw and think pair share.*
>
> **NAMNA YA KUTUMIA MUHTASARI HUU:** Katika muhtasari huu, mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji imependekezwa. Hata hivyo, mwalimu anatarajiwa kufanya uamuzi na ikiwezekana kutumia mbinu mseto kukuza ufundishaji. Kuna mbinu na taratibu ambazo zimependekezwa katika muhtasari huu ili kumwezesha mwalimu kufasiri muhtasari kwa urahisi. Baadhi ya mbinu ambazo zimependekezwa ni chemshabongo, majadiliano, maigizo, ujifunzaji wa kimakundi, uvumbuzi elekezi, na ushirikishaji wa wajifunzaji wawiliwawili (Tafsiri ni ya waandishi).

Kwa kurejelea dondoo hili, inabainika kwamba tafsiri ambayo inatumiwa kwa kiwango cha juu katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda kidato cha kwanza (*S1*) na cha pili (*S2*), haitambuliwi kama mbinu mojawapo. Pia, hakuna utafiti ambao umefanywa kuchunguza suala hili.

### 3.1 Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili jijini Kampala


Kinadharia tafsiri inapingwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2 na LgK, ingawa kiutendaji tafsiri hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari jijini Kampala nchini Uganda. Ili kubaini kiwango ambacho mwalimu hutumia tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili, matokeo ya majibu ya wajifunzaji yalikuwa kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Kiwango cha Matumizi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili**

| Na. | Shule | Jumla ya Watoataarifa | Mara Nyingi | Mara Chache | Hatumii |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shule ya Kampala | **51** | 29 | 21 | 1 |
| 2. | Shule ya Kawempe Muslim | **71** | 61 | 10 | 0 |
| 3. | Shule ya Kibuli | **48** | 26 | 21 | 1 |
| 4. | Shule ya Lubiri | **52** | 32 | 20 | 0 |
| 5. | Shule ya Midland | **29** | 19 | 9 | 1 |
| 6. | Shule ya Muyenga | **16** | 16 | 0 | 0 |
| 7. | Shule ya Progressive Kitintale | **21** | 12 | 9 | 0 |
| | **JUMLA** | **288** | **195** | **90** | **3** |
| | **ASILIMIA** (%) | **100%** | **68%** | **31%** | **1%** |

**Chanzo:** Ngesu (2021:173)

Data hii inaonesha kwamba tafsiri hutumiwa kwa kiwango cha juu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda. Matokeo katika Jedwali Na. 2 yanaonesha kwamba kati ya wanafunzi 288, wanafunzi 195 sawa na 68%, walisema kwamba mwalimu hutumia tafsiri mara nyingi. Wanafunzi 90 sawa na 31%, walisema kuwa mwalimu hutumia tafsiri mara chache, na wanafunzi 3 tu sawa na 1%, walisema kwamba mwalimu hatumii tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili. Matokeo haya yanalingana na matokeo ya hojaji kwa walimu ambapo kati ya walimu 48, walimu 26, sawa na 54%, walisema kwamba tafsiri hutumiwa kwa kiwango cha juu, na walimu 8 sawa na 17%, walisema kuwa tafsiri hutumiwa sana (taz. Ngesu, 2020:81). Hivyo, matokeo haya yanadhihirisha kwamba tafsiri hutegemewa kama njia muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kuwa wajifunzaji hawana nafasi ya kupata ingizo kutoka katika jamii. Kielelezo Na. 3 kinaonesha mgawanyo wa asilimia ili kutoa muhtasari na kumrahisishia msomaji kuelewa:




***Kielelezo Na. 3:*** ***Maoni ya watoataarifa (wanafunzi) kuhusu kiwango cha matumizi ya tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili***

**Chanzo:** Ngesu (2021:174)

Data katika Kielelezo Na. 3 inaonesha kwamba 68% ya wanafunzi walisema kwamba tafsiri hutumiwa mara nyingi katika ufundishaji wa Kiswahili, (31%) ya wanafunzi walisema kuwa tafsiri hutumiwa mara chache, na (1%) walisema kwamba tafsiri haitumiwi. Hali hii inadhihirisha kwamba walimu hutegemea tafsiri kama njia muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili.


Kulikuwa pia na umuhimu wa kupata maoni ya wajifunzaji kuhusu matumizi ya tafsiri. Hivyo, swali la 8 liliuliza: *Unafurahia kusoma Kiswahili mwalimu akitumia njia gani anapofundisha?* Wajifunzaji walitakiwa kuchagua jibu moja kati ya*: kutumia Kiswahili pekee* na *kutumia tafsiri ya Kiswahili kwenda Kiingereza.* Matokeo yalikuwa kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na. 4:

**Jedwali Na. 4: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Njia Wanayofurahia Mwalimu Akiitumia katika Ufundishaji wa Kiswahili**

| Na. | Shule | Jumla ya Watoataarifa | Akitumia Kiswahili pekee | Akitumia Tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Shule ya Kampala | **51** | 1 | 50 |
| 2. | Shule ya Kawempe Muslim | **71** | 0 | 71 |
| 3. | Shule ya Kibuli | **48** | 3 | 45 |
| 4. | Shule ya Lubiri | **52** | 0 | 52 |
| 5. | Shule ya Midland | **29** | 0 | 29 |
| 6. | Shule ya Muyenga | **16** | 2 | 14 |
| 7. | Shule ya Progressive Kitintale | **21** | 3 | 18 |
| | **JUMLA** | **288** | **9** | **279** |
| | | **100%** | **3%** | **97%** |

**Chanzo:** Ngesu (2021: 182)

Kwa kurejelea data katika Jedwali Na. 4, inaonekana kwamba kati ya wanafunzi 288, walioshiriki kujaza hojaji, wanafunzi 279 sawa na 97%, walisema kuwa hufurahia kujifunza Kiswahili mwalimu akitumia tafsiri, na wanafunzi 9 tu sawa na 3%, walisema kwamba hufurahia kujifunza mwalimu akitumia Kiswahili pekee. Matokeo haya yanaonesha kwamba wanafunzi 279, sawa na 97%, ni wakazi asilia wa Uganda na hawana umilisi wa Kiswahili. Hivyo, matumizi ya tafsiri huwasaidia kukuza uelewa wa dhana za Kiswahili. Kielelezo Na. 5 kinaonesha mgawanyo wa asilimia.





***Kielelezo Na. 5:*** ***Maoni ya wanafunzi kuhusu njia inayowasaidia kuelewa***

**Chanzo:** Ngesu (2021:182)

Kwa kurejelea Kielelezo Na. 5, inadhihirika kwamba 97% ya wajifunzaji wa Kiswahili hufurahia mwalimu akitumia tafsiri anapofundisha Kiswahili. swali la 8 liliuliza: *Unafurahia kusoma Kiswahili mwalimu akitumia njia gani anapofundisha?* Wajifunzaji walitakiwa kuchagua jibu moja kati ya*: kutumia Kiswahili pekee* na *kutumia tafsiri ya Kiswahili kwenda Kiingereza*. Swali hili liliambatana na swali jingine huria ambalo liliwahitaji wajifunzaji kueleza kwa nini walichagua jibu walilochagua. Hivyo, wajifunzaji wengi (jumla 97%) waliosema hufurahia mwalimu akitumia mikakati ya tafsiri walikuwa na mengi ya kusema. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa sababu ya kupenda kujifunza kwa tafsiri na alijaza hojaji kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na. 6: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Kupendelea Kujifunza Kiswahili kwa Tafsiri**



Give reasons for your answer in the above question
Since we are kiswahili beginners, the teacher needs to translate to English because it is the language we understand most.

**Chanzo:** Ngesu (2021:183)

Mjifunzaji katika Kielelezo Na. 6 anasema:

> Kwa kuwa tunaanza kujifunza Kiswahili, mwalimu anahitaji kutafsiri kwenda Kiingereza kwa sababu ni lugha tunayoielewa zaidi (Tafsiri ya waandishi).

Dondoo hili linaonesha kwamba tafsiri huwasaidia wajifunzaji kuelewa kwa sababu walianza kusoma Kiswahili katika kidato cha kwanza. Mtoataarifa mwingine (mwanafunzi) alisema kama ifuatavyo:


8 Give reasons for your answer in the above question

Kiswahili is a foreign laguage to me. ........ freign

It is my first time to learn Kiswahili. ........

It ~~star~~ I understand English more ........

Katika dondoo hili, mwanafunzi anaeleza kwamba Kiswahili kwake ni LgK kwa vile ilikuwa mara yake ya kwanza kujifunza. Sababu nyingine zilizotolewa na watoataarifa (wajifunzaji) zinaoneshwa katika Jedwali Na. 6 lifuatalo:

**Jedwali Na. 6: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Sababu za Kufurahia Mwalimu Akitumia Tafsiri katika Ufundishaji Kiswahili**

| Na. | Sababu | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Wanafunzi wengi hawaelewi Kiswahili kwa kuwa hawakusoma shule ya msingi. | 256 | 89% |
| 2. | Wanakutana na Kiswahili shule ya sekondari. | 220 | 76% |
| 3. | Maneno mengine ya Kiswahili ni magumu. | 100 | 35% |
| 4. | Walianza kujifunza Kiingereza wakiwa wachanga hivyo wanakielewa. | 266 | 92% |
| 5. | Tafsiri hurahisisha mawasiliano na kuwafanya waelewe dhana za Kiswahili. | 288 | 100% |
| 6. | Hufurahia kusoma Kiswahili mwalimu anapotumia tafsiri. | 151 | 52% |
| 7. | Hurahisisha ujifunzaji wa msamiati wa Kiswahili. | 187 | 65% |
| 8. | Husaidia katika ulinganishaji wa Kiswahili na Kiingereza ili kuepuka kufanya makosa. | 147 | 51% |
| 9. | Huwapa msukumo wa kusoma Kiswahili. | 77 | 27% |
| 10. | Huwawezesha kukabiliana na maswali ya tafsiri katika mtihani. | 85 | 30% |
| 11. | Husaidia kukuza stadi za lugha. | 92 | 32% |
| 12. | Huwezesha kujifunza lugha mbili kwa wakati mmoja. | 44 | 15% |

**Chanzo:** Ngesu (2021:187)

Data katika Jedwali Na. 6 inaonesha kwamba wanafunzi wote 288 sawa na 100%, walisema kwamba huelewa somo la Kiswahili mwalimu akitafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kwa sababu tafsiri hurahisisha mawasiliano na kuwafanya kuelewa dhana za Kiswahili. Wanafunzi 266 sawa na 92%, walisema kuwa hufurahia tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kwa sababu walianza kujifunza Kiingereza wakiwa wadogo, hivyo, wanakielewa Kiingereza vizuri. Kwa sababu hii, tafsiri kwenda Kiingereza huwafaa katika kurahisisha mawasiliano. Pia, wanafunzi 256 ambao ni 89%, walisema kwamba wanafunzi wengi hawaelewi Kiswahili kwa

kuwa hawakukisoma katika shule ya msingi. Wanafunzi 220 sawa na 76%, walisema kuwa walianza kujifunza Kiswahili shule ya sekondari jambo linaloashiria kwamba Kiswahili ni LgK.

**4.0 Hitimisho**

Matokeo ya utafiti wa makala hii yanaonesha kuwa kama ilivyoelezwa awali, tafsiri kwa ujumla hutumika kwa kiwango cha juu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK jijini Kampala. Aidha, matokeo yanaonesha kwamba tafsiri haiwezi kuepukika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari hususani kidato cha kwanza na cha pili katika muktadha maalumu wa ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Matokeo haya ni muhimu kwa kuibua hali tofauti na inavyoelezwa na watafiti wa awali ambao huhusisha tafsiri na Lg1 tu. Hata waliopinga matumizi ya tafsiri mwishoni mwa karne ya kumi na tisa walidai kuwa tafsiri-sarufi ilichangia athari hasi ya Lg1 katika ujifunzaji wa lugha. Makala hii inaonesha matokeo katika mazingira ambapo Lg2 hutumiwa katika ufundishaji wa Lg2/LgK.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yameweza kutengua mtazamo kwamba tafsiri haifai kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Imebainika kwamba tafsiri kwa ujumla ina nafasi yake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK jijini Kampala kutokana na kuwapo kwa mazingira ambayo wajifunzaji hawapati ingizo kutoka katika jamii. Makala hii imechangia katika mjadala mkuu unaoendelea kuhusu nafasi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za kigeni kwa kuonesha ushahidi wa kiutafiti kuwa tafsiri ni nyenzo mojawapo muhimu ya kufundisha na kujifunzia lugha za kigeni.

Pia, tafsiri ilionekana kuwapa motisha wajifunzaji na kuwasaidia kukabiliana na mihemko ambayo inaweza kuwa na athari hasi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK. Hali hii imetokana na sababu kwamba wanafunzi hawaelewi wakifundishwa kwa Kiswahili pekee kwa kuwa baadhi yao hawakujifunza Kiswahili katika shule ya msingi, wanafunzi hawapati ingizo kutoka nyumbani na katika mazingira ya nje ya darasa na Kiswahili ni LgK nchini Uganda. Hivyo, imebainika kwamba katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK jijini Kampala, matumizi ya tafsiri hayawezi kuepukwa kwa kidato cha kwanza na cha pili.

**5.0 Mapendekezo**

Kuna haja ya kutambuliwa kwa tafsiri kama mbinu mojawapo ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika mtaala na muhtasari wa ufundishaji hususani katika miktadha maalumu ambapo lugha hii haizungumzwi na wanajamii wengi. Imebainika kwamba licha ya tafsiri kutumika kwa kiwango cha juu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari, mbinu hii haitambuliwi katika mtaala kama mbinu mojawapo ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Mpaka sasa tafsiri hutahiniwa tu kama kipengele kimojawapo cha lugha. Kutambuliwa kwa tafsiri kama mbinu mojawapo ya

ufundishaji wa Kiswahili katika mazingira maalumu kutafanikisha kuratibu matumizi yake kwa mafanikio zaidi badala ya kuwaacha walimu kuitumia bila utaratibu wowote.

Pia, imebainika kwamba umilisi wa lugha mbili pekee hauwezi kufanikisha tafsiri mwafaka. Walimu katika shule za sekondari nchini Uganda wanahitaji warsha na semina za mara kwa mara ili kuboresha ufundishaji wa Kiswahili wanapotumia tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili.

Aidha, katika vyuo vikuu, ni muhimu mitaala ya Kiswahili kuwa na kozi ya tafsiri na kuhakikisha kuwa inafundishwa kama kozi ya lazima, yaani kozi tatu katika ngazi ya digrii ya kwanza, kozi mbili katika ngazi ya umahiri na kuendelea. Pia, mada ya mikakati ya tafsiri ni muhimu itiliwe maanani katika ufundishaji na ujifunzaji wa kozi za tafsiri kwa kuwa mikakati ya tafsiri ni suala la msingi katika mchakato wa tafsiri.

## Marejeleo


Abdul-Azim, H.O.M. (2017). "*Use of Translation for Enhancing Learning Performance of Students at the University Level*." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Sudani cha Sayansi na Teknolojia. Sudani. Inapatikana katika http://repository.sustech.edu/handle/123456789/20410. Ilisomwa tarehe 11 Mei 2018.

Anwar, W.P. (2019). *Exploring Translanguaging: An Approach to Teaching and Learning English as Foreign Language of Bone Islamic University Context.* Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Negeri Makassar, Indonesia Inapatikana katika http://eprints.unm.ac.id/ 14952/1/ARTIKEL.pdf. Ilisomwa tarehe 13 Oktoba 2019.

Ayvazyan, N. (2017). *Communicative Translation in Foreign-Language Teaching and Learning*. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Universitat Rovira Virgili. Inapatikana katika https://scholar.google.com/scholar. Ilisomwa tarehe 11 Mei 2019.

Bloomfield, L. (1933). *Language*. New York: Holt and Co.

Celce-Murcia, M. na Rosensweig, F. (1979). "Teaching Vocabulary in the ESL Classroom". *Teaching English as a Second or Foreign Language*, Juz. 6: 241-257.

Cook, G. (2010). *Translation in Language Teaching: An Argument for Reassessment*. Oxford: Oxford University Press.

Cook, V. (2013). *Second Language Learning and Language Teaching*. London and New York: Routledge. Inapatikana katika Routledgehttps://books.google.co.tz/books. Ilisomwa tarehe 16 Oktoba 2017.

Cook, G. (2018). "Learning Through Translation". Katika Burns, A. & Richards, J.C. (Wahr.), *The Cambridge Guide to Learning English as a Second Language* London: Cambrigde University Press. Kur. 289-306.

Dagilienė, I. (2012). "Translation as a Learning Method in English Language Teaching". *Kalbų studijos*, Juz. 21: 124-129.

Doff, S. (2008). "How Language Teaching Started Afresh: Origins and Repercussions in the Reform Movement in German Foreign Language Teaching Curricula". *Journal of the American Association for the Advancement of Curriculum Studies*, Juz. 4:1-16 Inapatikana katika https://ojs.library.ubc. ca/index.php/jaaacs/article/view/187672/185771. Ilisomwa tarehe 17 Januari 2020.

Fitori, H.S.O. (2019). Difficulties *in Teaching and Learning English Grammar in Libyan Universities.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Liverpool John Moores. Inapatikana katika https://researchonline.ljmu. ac.uk/id/eprint/10991. Ilisomwa tarehe 15 Mei 2020.

Howatt, A.P.R. (1984). "Language Teaching Traditions: 1884 Revisited". *ELT Journal*, Juz. 38 (4): 279-282.

Hull, T. (2018). "Content Based Instruction: A communicative Approach for the EFL Classroom". *PUPIL. International Journal of Teaching, Education and Learning*, Juz. 2(3): 63-77.

Ito, K. (2017). *The Efficacy of Translation and Oral Corrective Feedback in Promoting Language Proficiency Development*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). State University of New York at Binghamton. New York. Inapatikana katika https://www.proquest.com/openview/a1d57456f666b23a8cd642791497ace8/1?pq-origsite=gscholar&cbl=18750&diss=y. Ilisomwa tarehe 11 Mei 2018.

Ivanova, I. (2016). "Re-introducing Own-language Use, Code-switching and Translation in FL Classrooms through Intralingual Strategies and Approaches." *Eltam Journal*, Juz. 9: 5-16.

Jjingo, C. (2011). *Language Policy and the Promotion of Kiswahili in Uganda.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Jjingo, C. na Visser, M. (2017). "The Ssenteza Kajubi Legacy: The Promotion of Teaching Kiswahili in Uganda". *Journal of Pan African Studies*, Juz. 10(9): 1-14.

Jjingo, C. na Visser, M. (2018). "Exploring a Forward Design Dimension in the Design of School-based Kiswahili Teaching syllabus for Primary Schools in Uganda. *Per Linguam". A Journal of Language Learning Per Linguam: Tydskrif vir Taalaanleer*, Juz. 34(2): 84-96.

Karimah, A. (2020). “Revisiting Translation as a Foreign Language Learning Tool: Contrasting Beliefs of Diversely Proficient Students”. *Saga: Journal of English Language Teaching and Applied Linguistics*, Juz. 1(1): 9-16.

Liu, G. (2019). “Language Sociality and Its Enlightenment on Foreign Language Teaching”. *Theory and Practice in Language Studies*, Juz. 9(8): 978-983.

Machida, S. (2011). “Translation in Teaching a Foreign (Second) Language: A Methodological Perspective”. *Journal of Language Teaching & Research*, Juz. 2(4): 740-746.

Majariwa, D. (2014). *The Role of Kiswahili Pedagogy in Developing the Communicative Competence of ‘O’ Level Students: A Case Study of Mbarara Municipality Schools*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Makerere. Kampala.

Marqués A.T. na Solís-Becerra, J. A. (2013). “An Overview of Translation in Language Teaching Methods: Implications for EFL in Secondary Education in the Region of Murcia”. *Revista de Lingüística y Lenguas Aplicadas*, Juz. 8(1): 38-48.

Masengo, I.J. (2018). *Cross-linguistic Influence in Third Language Production among Kiswahili Learners*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Makerere. Kampala.

Michira, J.N. na Indindi, H. (2019). “Uchanganuzi wa Tafsiri za Kiwavuti katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama LgK: Mfano wa *Google Translate”*. *Jarida la Kimataifa la Isimu ya Kibantu*, Juz. 2: 62-79.

Ministry of Education & Sports. (2008). *Revised Education Sector Strategic Plan 2007-2015*, Kampala.

Ministry of Education and Sports. (2008). *Kiswahili Teaching Syllabus.* Uganda National Curriculum Development Center. Kampala.

Mtesigwa, P. (2009). “Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama LgK: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Mawasiliano”. *Kiswahili*, Juz. 72(1): 52-67.

Ngesu, S.N.M. (2021). Tafsiri katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni nchini Uganda. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Ngesu, S.N.M. (2020). “Nafasi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili: Mfano wa Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili nchini Uganda.” *Jarida la Mwanga wa Lugha*, Juz. 7(1): 71-88.

Ngesu, S.N.M. (2018). “Issues of Language Structure in Machine Translation: A Case Study of English and Kiswahili”. Katika Sin-wai (Mhr.), *The Human Factor in Machine Translation.* New York and London: Routledge. Kur. 153-182.

Nida, E.A. (1998). “Language, Culture and Translation”. *Foreign Languages Journal*, Juz. 115(3): 29-33.

Ninsiima, B. (2017). *Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi wa Sekondari Wanapotafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Omaggio, H.A. (2001). *Language Teaching in Context*. Boston: Heinle.

Omar, Y.Z. (2019). "Influence of Grammar Translation Method (GTM) on Libyan Students English Performance in Communicative Situations". *People: International Journal of Social Sciences*, Juz. 5(2): 511-530

Philipo, Z.T. (2016). "Dhima ya Tafsiri katika Ufundishaji na ujifunzaji wa LgK/ Pili: Mfano Lugha ya Kiswahili". Katika Jilala (Mhr.), *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited. kur. 420-437.

Pintado, G.L. (2018). "Translation in Language Teaching, Pedagogical Translation, and Code-Switching: Restructuring the Toundaries". *The Language Learning Journal*, Juz. 1: 1-21.

Pym, A. na Ayvazyan, N. (2017). "Linguistics, Translation and Interpreting in Foreign-Language Teaching Contexts". *The Routledge Handbook of Translation Studies and Linguistics*, Juz. 1: 393.

Siefert, T.R. (2013). Translation *in Foreign Language Pedagogy: The Rise and Fall of the Grammar Translation Method*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Harvard. Inapatikana katika https://dash.harvard.edu/handle/1/10952296. Ilisomwa tarehe 10 Septemba 2019.

Vermes, A. (2010). "Translation in Foreign Language Teaching: A Brief Overview of Pros and Cons". *Eger Journal of English Studies*, Juz. 10: 83-93. Viëtor, W. (1902). *Die Methodik des neusprachlichen Unterrichts: Ein geschichtlicher Überblick in vier Vorträgen*. Leipzig: B.G. Teubner.